# MKATABA WA NAIROBI WA HIFADHI, USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA MAZINGIRA YA BAHARI NA UKANDA WA PWANI YA MAGHARIBI YA BAHARI YA HINDI

## 1. UTANGULIZI

Mkataba wa Nairobi Kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi *(Convention for the Protection, Management, and Development of the Marine and Coastal Environment of the Eastern African Region)* ulipitishwa tarehe 21 Juni, 1985. Tanzania iliridhia Mkataba huu tarehe 1 Machi, 1996. Aidha, Mwaka 1999 Mkataba huu ulifanyiwa marekebisho ambapo Tanzania iliridhia marekebisho hayo tarehe 4 Septemba, 2017. Mkataba huu una jumla ya Nchi Wanachama kumi (10) ambazo ni: Komoro, Kenya, Somalia, Madagascar, Mauritius, Msumbiji, Shelisheli, Re-Union – Ufaransa, na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Afrika Kusini.

## 2. Lengo la Mkataba

Lengo kuu la Mkataba huu ni kudhibiti uchafuzi wa mazingira ya ukanda wa pwani na bahari kutokana na vyanzo na shughuli zinazofanyika nchi kavu. Aidha, Mkataba unalenga kuwezesha nchi wanachama, kushirikiana katika kuandaa mipango na mikakati ya pamoja katika kuhifadhi, kusimamia na kuendeleza mazingira ya ukanda wa pwani na bahari.

## 3. Itifaki zilizo chini ya Mkataba wa Nairobi

Mkataba wa Nairobi una jumla ya Itifaki nne (4) ambazo ni;

i. Itifaki kuhusu Maeneo Tengefu na Wanyamapori na Mimea katika Ukanda wa Afrika Mashariki 1985 (Itifaki hii ipo kwenye marekebisho - mazungumzo ya mwisho ya nchi wanachama yalifanyika 2025 nchini Madagaska) *"Protocol concerning Protected Areas and Wild Fauna and Flora in the Eastern African Region - 1985" (this is now being amended - last negotiations were done 2025 in Madagascar);*
ii. Itifaki ya Usimamizi Shirikishi wa Ukanda wa Pwani katika Kanda ya Magharibi ya Bahari ya Hindi *"Protocol on Integrated Coastal Zone Management in Western Indian Ocean Region (ICZM)-2023";* Tanzania ilisaini itifaki hii mnamo tarehe 12 Septemba, 2023 nchini Madagascar;
iii. Itifaki inayohusu Ushirikiano katika Kupambana na Uchafuzi wa Bahari katika Matukio ya Dharula katika Ukanda wa Afrika Mashariki 1985

"*Protocol Concerning Co-operation in Combating Marine Pollution in Cases of Emergency in the Eastern African Region - 1985"; na*

iv. Itifaki ya Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi Kutokana na Vyanzo na Shughuli Zinazofanyika Nchi Kavu ***"****Protocol for the Protection of the Marine and Coastal Environment of the Western Indian Ocean from Land-Based Sources and Activities - 2010 (LBSA protocol)".*

## 4. Ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mikutano ya Nchi Wanachama (COP)

Mikutano ya nchi wanachama (COP) hufanyika kila baada ya miaka miwili, Sekretarieti ya Mkataba wa Nairobi huandaa mikutano hiyo kwa kushirikiana na Kamati tendaji (Bureau to the Nairobi Convention Secretariat). Lengo ni kuwezesha Nchi Wanachama kujadili kwa pamoja kuhusu mafanikio na changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika utekelezaji wa Mkataba wa Nairobi na Itifaki zilizopo chini ya Mkataba huu.

## 5. Mafanikio ya utekelezaji wa mkataba

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na kuridhia Mkataba huu ni pamoja na:-

i. Upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi mbalimbali kwa ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP) kupitia Sekretarieti ya Mkataba wa Nairobi pamoja na washirika wa maendeleo;
ii. Kuimarisha ushirikiano wa kikanda na nchi zingine za ukanda wa Magharibi mwa bahari ya hindi katika nyanja ya hifadhi, usimamizi na uendelezaji wa mazingira ya bahari na ukanda wa pwani ya magharibi mwa bahari ya hindi;
iii. Utekelezaji wa miradi ya hifadhi ya mazingira ya bahari na ukanda wa pwani ukiwemo mradi wa mfano wa Wilaya ya Mkinga utakaotumiwa na nchi zote wanachama wa Mkataba wa Nairobi kujifunza na hivyo kuchangia katika jitihada za maendeleo na upatikanaji wa huduma nchini;
iv. Kupata fursa ya kuwa sehemu ya utekelezaji wa mradi wa kuzuia uchafuzi kwa unaotokana na plastiki unaosimamiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP) ambapo Tanzania itapata fursa katika kujenga uwezo wa kitaasisi juu ya kuzuia uchafuzi unaotokana na plastiki na kuongezewa muda wa utekelezaji wa mradi wa kuzuia uchafuzi wa mazingira ya bahari unaotokana na taka za plastiki *"Marine Litter Project"* hadi kufikia Julai, 2025 pamoja na kiasi cha fedha kutoka Dola za Kimarekani 110,000 hadi kufikia 210,000;
v. Kuandaa Mikakati ya kuhifadhi mazingira ya bahari kama vile National Oil Spills Response Contigency Plan, na taarifa za hali ya Maeneo hayo kama vile Matumbawe;

vi. Kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira ya bahari, faida zake na athari za kutofanya hivyo; na
vii. Kuwa Mwenyekiti wa Kamati tendaji ya Mkataba wa Nairobi *(Chair of the Bureau to the Nairobi Convention)* kwa kipindi cha Miaka Miwili (2) hadi mwaka 2026.
viii. Fursa ya kubadilishana uzoefu na utaalam kuhusu masuala ya hifadhi ya bahari, ukanda wa pwani pamoja na Uchumi wa Buluu.

### 6.2 Changamoto za utekelezaji wa mkataba

Utekelezaji wa mkataba huu unakabiliwa na changamoto kadhaa, hasa katika kushughulikia masuala ya Usimamizi na uendelezaji wa mazingira ya Pwani ya bahari kama ifuatavyo;

i. Ongezeko la uchafuzi wa mazingira ya bahari unaotokana na shughuli mbalimbali; ikiwemo taka zisizotibiwa, mtiririko wa mabaki yatokanayo na kilimo, uchafuzi uanotokana na taka za plastiki na uchafuzi wa taka za viwandani zinazoelekezwa baharini.
ii. Ukosefu wa takwimu na ufuatiliaji hali ambayo huzuia usimamizi bora wa mifumo ya ikolojia ya baharini.
iii. Mabadiliko ya taabianchi, ambapo vyanzo mbalimbali vimekuwa vikibainisha kuongezeka kwa mmomonyoko ardhi katika maeneo ya wa pwani kwa kiwango kikubwa unaotishia mifumo ikolojia.

### 6.3 Hatua za Utatuzi wa Changamoto

i. Kuimarisha na kusimamia udhibiti wa uchafuzi wa mazingira ya bahari utokanao na taka zitokazo nchi kavu, inayojumuisha usimamizi jumuishi wa ukanda wa pwani ya bahari ya hindi;
ii. Kuimarisha mifumo ya takwimu ili kujua ukubwa wa tatizo pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kikanda; na
iii. Kurejesha uoto na miundombinu ya asili kama vile; nyasi, misitu ya mikoko, matumbawe, mawe pamoja na ujenzi wa miundombinu mingine kama ujenzi wa kuta katika baadhi ya maeneo ili kuzuia mmomonyoko wa ardhi na fukwe katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani.

## 6. HITIMISHO

(OMR) itaendelea kusimamia Mkataba huu kwa ufanisi ili kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika kuratibu uhifadhi wa Mazingira ya Bahari ya Hindi na kuwezesha nchi kunufaika na rasilimali ya bahari katika eneo husika na kupata fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya usimamizi na uendelezaji wa mazingira ya bahari kwa ukanda wa pwani ya magharibi ya Bahari ya hindi. Aidha, kuwezesha nchi kunufaika na fursa

za kujenga uwezo kitaasisi na kitaalamu katika kusimamia, kuhifadhi na kuendeleza mazingira ya Bahari ya Hindi na ukanda wa pwani.